



WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA WANANCHI KUHUSU KUANZA KWA SHUGHULI ZA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR

IMETOLEWA NA WAZIRI WA AFYA

MHE. NASSOR AHMED MAZRUI

TAREHE 30/6/2023

Ndugu Wananchi;

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Afya inaendelea na jitihada za kuhakikisha, inawapatia wananchi wake huduma bora za afya. Katika kufanikisha juhudhi hizo, Serikali ya Awamu ya Nane chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, imeanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar kupitia Sheria Na. 1 ya mwaka 2023.

Ndugu Wananchi;

Kifungu cha 2 (1) (a), (b), (c), (d), (e) na (f) cha Sheria hiyo, kinatoa ulazima kwa wananchi na wakaazi wote wa Zanzibar kujunga na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar. Utekelezaji wa takwa hili la kisheria utakuwa kwa awamu kama ilivyoelizwa katika kifungu cha 2 (2) na (3). Kifungu cha 2(2) kinaeleza kwamba utekelezaji wa Sheria hii utaanza kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na sekta binafsi, ambao watajisajili na kuwa wanachama wa Mfuko mara baada ya Sheria hii kuanza kutumika.

Hivyo, naomba kuwatangazia waajiri na waajiriwa wote wa sekta ya umma na binafsi kuanza kufanya usajili ifikapo tarehe 3 mwezi Julai 2023 kupitia Tovuti ya Mfuko www.zhsfsmz.go.tz na kufuata maelekezo yaliyopo pamoja na kupata usaidizi kupitia barua pepe ya Mfuko info@zhsfsmz.go.tz au kufika katika Ofisi za Mfuko Michezani Mall Wing C Ghorofa ya Nne chumba namb. 401 na 402.

Ndugu Wananchi;

Kutakuwa na muda wa kusubiri kabla ya kupata huduma kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 25 cha Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar. Kipindi hiki kitakuwa cha miezi mitatu kuanzia Julai 2023 hadi Septemba 2023. Katika kipindi hiki, Michango itakuwa inakusanywa kutoka kwa wanachama na waajiri wa Sekta ya Umma na Binafsi huku wakiendelea kupata huduma za Afya bure katika vituo vyote vya Umma.

Ndugu Wananchi;

Katika kufikia huduma bora kwa wananchi, Serikali tayari imeweka uwekezaji mkubwa katika Ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Mkoa. Tunadhamira kwa dhati kufanya mabadiliko makubwa katika usimamizi wa Hospitali hizo ili huduma ziwe bora. Nipende pia kusisitiza sekta binafsi kuitumia fursa hii kushirikana na Serekali katika kuimarisha huduma za Afya nchini.

Ndugu Wananchi;

Kwa wale wafanyakazi wa Sekta zilizopo Zanzibar ambao vituo vyao vya kazi viro Tanzania Bara au wakaazi wa Zanzibar ambao watakuwa Tanzania bara kwa dharura, na wakawa na uhitaji wa kupata huduma za afya, Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar utaandaa utaratibu mahsus kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya(NHIF) kuweza kutumia mtandao wao wa Watoa huduma za Afya kuwawezesha wanachama kupata huduma hizo wakiwa Tanzania Bara. Ni dhana ambayo hata katika Jumuia ya Afrika Mashariki inazungumzwa kuwawezesha wanachama wa Mifuko ya Nchi hizo wanaposafiri nje ya Nchi zao kupata huduma hizo kuititia Mifuko ya Nchi zao.

Ndugu Wananchi;

Naomba kutoa ufanuzi kwamba:

- Ijapokua kujeungu na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar ni lazima, haiondoshi fursa ya mwananchi ambae anauwezo wa kifedha kujeungu na utaratibu mwengine. Mwananchi anaweza kupata huduma za ziada kwa Taasisi nyengine zilizopo kwa mujibu wa sheria. Aidha, Mfuko utakapo imarika, utaweza pia kutoa huduma nyengine za ziada nje ya kitita cha huduma za Mfuko kilichoainishwa katika Jaduweli la Tatu la Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar Nam. 1 ya 2023.
- Katika kipindi hiki cha mpito, wafanyakazi wanaweza kuendelea kuchangia NHIF kwa hiari na kuendelea kupata huduma hadi Septemba 2023 kabla ya kuanza kwa huduma za Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar Oktoba 1, 2023.

Ndugu Wananchi;

Nawaomba wananchi wote watoe ushirikiano wa hali ya juu ili kufanikisha hili.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza na Nawatakia kila la Kheri.



**NASSOR AHMED MAZRUI,
WAZIRI WA AFYA,
ZANZIBAR.**